JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI
Ofisi ya Meneja wa Wilaya, S. L. P. 330 Kyela.
Tovuti: www.ruwasa.go.tz Barupepe: kyeladm@ruwasa.go.tz

Unapojibu Tafadhali Taja
Kumb. Na. RUW/KYE/NKY/VOL-1/13 04/4/2024

# TANGAZO LA NAFASI (4) ZA KAZI YA WASIMAMIZI (SUPERVISOR) NA NAFASI (4) ZA WAHASIBU WA VYOMBO VYA WATOA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII VYA MTM, KAPAPA, NGAMANGA NA NDOMAMA

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kyela kwa niaba ya vyombo vya watoa huduma za maji ngazi ya jamii vya MTM, KAPAPA, NGAMANGA NA NDOMAMA anatangaza nafasi za kazi za Wasimamizi (Supervisors) na Wahasibu wa Vyombo vya MTM, KAPAPA, NGAMANGA NA NDOMAMA.

Nafasi 4 za Wasimamizi (supervisor)
Nafasi 4 za Wahasibu

Waombaji wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

1. MSIMAMIZI WA CHOMBO (SUPERVISOR)

**Sifa za Mwombaji:**

a) Awe ni Mtanzania mwenye akili timamu anayejua kusoma na kuandika
b) Awe na cheti cha ufundi sanifu NTA 3 na kuendelea
c) Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
d) Awe mwadilifu, mwaminifu na hajahukumiwa kwa kosa la jinai
e) Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kuhitaji usimamizi mkubwa
f) Awe na uwezo wa kusimamia wafanyakazi wengine
g) Awe na uwezo wa kubuni, kuanzisha na kuendeleza huduma ya maji

**Majukumu ya Msimamizi wa Chombo (Supervisor)**

a) Atafanya kazi chini ya Kamati ya maji ya Chombo na atakuwa katibu wa kamati hiyo
b) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu na Msimamizi wa waajiriwa wengine katika Chombo
c) Atatoa mapendekezo na makisio ya mapato na matumizi ambayo yatajadiliwa na Kamati ya Maji ya Chombo
d) Atatekeleza kazi za Chombo atakazopangiwa na kamati ya Maji ya Chombo.
e) Atasimamia utoaji wa huduma ya maji yenye viwango vya ubora kwa watumiaji maji
f) Ataandaa taarifa za uendeshaji wa mradi kila wiki, kila mwezi, kila robo, kila nusu mwaka na kila mwaka na kuziwasilisha kwenye vikao vya Kamati ya Maji ya Chombo na kwa Meneja wa Wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Kyela.
g) Atasimamia matengenezo ya mradi na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Kamati ya Maji ya Chombo na kwa Meneja wa RUWASA Wilaya Kyela
h) Ataandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti, mapato na matumizi
i) Atahamasisha uchangiaji wa huduma ya maji, kutatua na kusuluhisha migogoro baina ya watumiaji wa maji na Chombo na wadau wengine.
j) Atafanya manunuzi ya mahitaji ya mradi kwa kufuata taratibu za manunuzi ya umma

2. MHASIBU WA CHOMBO

**Sifa za Mwombaji:**

a) Awe ni Mtanzania mwenye akili timamu
b) Awe na elimu ya cheti cha uhasibu NTA 3 na kuendelea.
c) Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
d) Awe muadilifu, mwaminifu na hajahukumiwa kwa kosa la jinai
e) Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kuhitaji usimamizi mkubwa

**Majukumu ya Mhasibu wa Chombo:**

a) Atafanya kazi chini ya Msimamizi wa Chombo (supervisor)
b) Atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya fedha katika Chombo
c) Atapokea malipo ya maji na michango ya wanachama, na feha toka kwa wadau wengine.
d) Ataandaa taarifa ya mapato na matumizi kwa vipindi vya kila robo yaani miezi mitatu mitatu.

e) Atatoa tafsiri ya nyaraka na kumbukumbu za hesabu za Chombo pale atakapohitajika kufanya hivyo
f) Atatunza vitabu vya fedha, hati za malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa manunuzi, mapato, malipo au matumizi ya fedha
g) Atafanya malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Chombo
h) Atatunza daftari (Regista) ya wateja wote wa huduma ya maji

3. MASHARTI YA JUMLA NA POSHO/MSHAHARA
   a) Malipo yatatokana na makusanyo au mauzo ya maji ya Chombo husika
   b) Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika mazingira ya vijijini na awe tayari kupangiwa katika Chombo chochote kile

4. MELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

   Mwombaji aandike barua ya maombi kwa mkono akielezea ni kwa nini anadhani yeye anafaa kwa kazi husika na aweke viambatisho vifuatavyo:-

   a) Nakala ya vyeti vya elimu, taaluma na/au ujuzi alionao

   b) Nakala ya kitambulisho cha uraia au kadi ya mpiga kura au cheti cha kuzaliwa

   c) Majina na mawasiliano ya wadhamini wake

Maombi yaliyofungwa vizuri kwenye bahasha yatumwe kwenda anuani ifuatayo:-

**MENEJA WA RUWASA**
**WILAYA YA KYELA**
**S. L. P. 330**
**KYELA**

Pia maombi hayo yanaweza kutumwa kwa njia ya baruapepe ya: **kyeladm@ruwasa.go.tz** nyingine ni: **tdeule@yahoo.co.uk.** Aidha maombi yanaweza kuwasilishwa kwa mkono katika Ofisi ya Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kyela iliyopo Kyela mjini eneo la Mpanda bwawani

kwenye jengo la ofisi ya Elimu Sekondari kuanzia saa 2 asbuhi hadi saa 11.00 jioni Jumatatu hadi Ijumaa au Maombi hayo pia yanaweza kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Chombo cha MTM (0762643449/0655463449), Mwenyekiti wa Chombo cha NGAMANGA (0742158293/0712622232), Mwenyekiti wa Chombo cha KAPAPA (0787558480), Mwenyekiti wa chombo cha NDOMAMA (0783320122),

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Jumatatu tarehe 06/05/2024 saa 11.00 Jioni.**

Tangazo hili limetolewa na:-

Eng Deule, T.
**MENEJA RUWASA (W)**
**KYELA**

MENEJA WA RUWASA
KYELA

**Nakala:**

Mbao mbalimbali za matangazo na Mitandao ya Kijamii
KYELA